HALMASHAURI YA WILAYA YA KILWA

MPANGO WA USIMAMIZI WA MSITU

KIJIJI CHA KISANGI

MPANGO UMEANDALIWA NA SERIKALI YA KIJIJI CHA

KISANGI

MWAKA 2007

YALIYOMO

1: UTANGULIZI 3
1.1 Umiliki wa msitu 3
1.2 Lengo kuu la Mpango wa Usimamizi 3
1.3 Madhumuni 3
1.4 Muda 3

2: HISTORIA FUPI YA MPANGO KAZI 4
2.1 Jamii 4
2.2 Maelezo kuhusu Msitu 4
2.2.1 Mahali ulipo Msitu na ukubwa wake 4
2.2.2 Uoto wa asili na Mazingira. 4
2.2.3 Rasilimali za misitu. 4
2.2.4 Jamii za miti ya mbao 5
2.2.5 Mazao yasio timbao 5
2.2.6 Wanyama pori. 5
2.2.7 Mambo ya asili & Haki za kijadi 5
2.2.8 Historia ya nyuma 5
2.2.9 Matumizi ya sasa 5

3: MWONGOZO WA MATUMIZI YA MAZAO YA MISITU 6
3.1 Matumizi ya msingi 6
3.2 Matumizi huru ya msitu 6
3.3 Shughuli katika misitu zitakazotozwa ushuru 6
3.4 Mazao yanayohitaji vibali vya uvunaji 6
3.4.1 Utaratibu wa kupata leseni ya uvunaji 7
3.5 Matumizi yasiyoruhusiwa ndani ya msitu 7

4: HAKI, MANUFAA NA MAJUKUMU YA WADAU 8
4.1 Kijiji 8
4.1.1 Haki 8
4.1.2 Manufaa 8
4.1.3 Majukumu ya Serikali ya Kijiji 8
4.1.4 Majukumu ya Kamati ya Maliasili 8
4.1.5 Majukumu ya Wanakijiji 9
4.2 Halmashauri ya Wilaya 9
4.2.1 Haki 9
4.2.2 Manufaa 9
4.2.3 Majukumu ya Halmashauri ya Wilaya 9
4.3 Majukumu ya Serikali Kuu 10

5: SHUGHULI ZA KUENDELEZA NA KUTUNZA MSITU 11
5.1 Mikakati ya jumla ya kuendeleza msitu. 11
5.2 Ulinzi wa msitu 11
5.2.1 Ushirikishwaji wa jamii katika ulinzi wa msitu. 11
5.2.2 Walinzi wa doria 11
5.3 Kusafisha mpaka na barabara za moto 12

6: MAPATO NA USIMAMIZI WA MAZAO YA MSITU 13
6.1 Vyanzo vya mapato 13
6.2 Mgawanyo wa Mapato kwa Wadau 13
6.3 Ukusanyaji na Utunzaji wa Fedha 13
6.3.1 Vitabu muhimu vya kutunza kumbukumbu vinavyotakiwa 14
6.3.2 Taarifa ya Mapato na Matumizi 14
6.3.3 Kuwajibishwa 14

7: UFUATILIAJI NA TATHIMINI 15
7.1 Ufuatiliaji 15
7.2 Tathimini ya kati na ya mwisho 15

KIAMBATISHO A : RAMANI ZA KIJIJI NA MSITU 16
Ramani inayoonyesha mipaka ya Kijiji 16

Ramani inayoonyesha mipaka ya Msitu wa Kijiji *17*
Ramani Shirikishi ya Kijiji *18*

KIAMBATISHO B : MPANGO WA UTEKELEZAJI **18**

Kazi za kila mwaka *18*
Kazi za Mwaka wa Kwanza *19*
Kazi za Mwaka wa Pili *19*
Kazi za Mwaka wa Tatu *19*

KIAMBATISHO C : VIWANGO VYA USHURU **19**

SURA YA KWANZA

1: UTANGULIZI

Sera ya Taifa ya Misitu ya mwaka 1998 inatoa kipaumbele kwa jamii kushirikishwa katika usimamizi wa misitu. Pia sera inasisitiza mchango wa sekta ya misitu katika kukuza kipato cha jamii ili kupunguza umasikini. Mwaka 2002 serikali ya Tanzania ilipitisha sheria mpya ya misitu ambayo inazipa jamii zinazoishi kandokando ya misitu mamlaka ya kusimamia misitu yao.

Kijiji cha Kisangi kimeandaa mwongozo wa matumizi endelevu kwa Msitu wa Kijiji. Matumizi haya yameainishwa katika mpango kazi huu. Mpango huu umefafanua na kuweka bayana shughuli zote zitakazofanyika katika kipindi cha kutumika kwa mpango zikiwemo shughuli za uboreshaji wa msitu, utaratibu wa usimamizi, udhibiti wa uhalifu wa msitu, mapato na matumizi yatokanayo na rasilimali za msitu, ukusanyaji na usimamizi wa mapato yatokanayo na msitu na Utunzaji wa kumbukumbu za matukio mbalimbali yatokanayo na msitu. Ili masharti ya matumizi ya msitu yaweze kufuatwa ipasavyo, kijiji kimetunga sheria ndogo za utunzaji wa msitu ambazo zimewekwa kama kiambatanisho kwenye mpango huu.

Rasimu ya mpango shirikishi imeandaliwa na kamati ya maliasili ya kijiji, wadau wa matumizi ya msitu, Serikali ya kijiji wakishirikiana na timu ya wataalamu na wawezeshaji kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa chini ya Mpango wa Taifa wa Usimamizi Shirikishi wa Misitu. Wawezeshaji toka Mradi wa Kuhifadhi Mpingo nao walishiriki katika kuandaa rasimu hii. Mpango huu utatumika katika kipindi cha miaka mitano.

1.1 Umiliki wa msitu

Msitu unamilikiwa na Serikali ya Kijiji cha Kisangi. Msitu wa Kijiji wa Kisangi ulitengwa kuwa hifadhi Mwaka 2005 chini ya usaidizi wa kitalaamu toka kwa wawezeshaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa na wawezeshaji wa Mradi wa Kuhifadhi mpingo.

1.2 Lengo kuu la Mpango wa Usimamizi

Msitu wa Kijiji ulitengwa kwa lengo la kuwa na uvunaji endelevu wa miti ya mbao, mazao yasiyo timbao na rasilimali zingine za misitu. Lengo kuu likiwa ni kuweka msitu katika hali ya uasilia na kuboresha hali ya maisha ya kizazi kilichopo na kijacho.

1.3 Madhumuni

- Kuhifadhi eneo la Msitu wa Kijiji cha Kisangi lenye ukubwa wa hekta 2,032 dhidi ya ukataji miti ovyo, uharibifu na matumizi yasiyofaa.
- Kijiji cha Kisangi kupata mapato kutokana na biashara ya rasilimali za misitu na hivyo kuchangia kuboresha hali ya maisha ya wanajamii.
- Kupunguza uvunaji holela wa mazao ya misitu.
- Kuhakikisha kuna upatikanaji wa mazao ya misitu.
- Kuwajengea wanajamii wa Kisangi uwezo wa kusimamia rasilimali za misitu asilia zilizopo Kijijini.

1.4 Muda

Huu ni mpango wa miaka mitano. Mpango huu utarekebishwa mwishoni mwa mwaka wa tatu au muda wowote endapo kuna umuhimu wa kufanya hivyo. Hakutafanyika mabadiliko yeyote katika mpango huu bila ya kibali cha Halmashauri ya Wilaya.

SURA YA PILI

2: HISTORIA FUPI YA MPANGO KAZI

2.1 Jamii

Kijiji cha Kisangi Kimbarambara kipo katika kata ya Kikole, tarafa ya Pwani, katika Wilaya ya Kilwa. Kinaitwa Kisangi tu kwa kifupi. Kina idadi ya watu wapatao 1,273 katika kaya zipatazo 210, na kina kilomita za mraba zipatazo 109km². Kijiji kilisajiliwa tarehe 7/8/1996, kabla kilikuwa kitongoji cha Ruhatwe.

Kijiji hiki kinapakana na vijiji vya Ruhatwe kwa upande wa kusini, Matandu kwa mashariki, Miteja kwa upande wa mashari-kaskazini, Nambondo kwa upande wa kaskazini na Kikole kwa upande wa magharibi.

Kijiji bado hakina Cheti cha ardhi cha kijiji, lakini mipaka inajulikana vizuri kwa sababu ni mipaka ya kale ya Ruhatwe, kaskazini ya Mto wa Matandu. Pia kijiji kina muhitasari wa makubaliano kuhusu mipaka pamoja na vijiji vyote vinavyopakana na Kisangi. Mipaka ya kijiji tayari imeshapimwa na imewekwa mawe ya alama. Angalia Kiambatisho A: Ramani ya Kijiji na msitu.

Vitongoji vya kijiji vinavyotambulika ni Kisangi na Mikulyungu. kati ya hivyo kitongoji cha Mikulyungu kiko karibu na Msitu wa Kijiji. Angalia KiambatishoA: mchoro wa ramani ya kijiji cha Kisangi.

2.2 Maelezo kuhusu Msitu

Msitu huu ni wa asili na watu waliishi kwenye baadhi ya maeneo machache miaka ya 1944 mpaka 1971. Hakuna shughuli yoyote ya kijadi inayofanyika katika eneo hilo. Pia msitu huu ni muhimu kwani vyanzo vya maji ya kunywa na chemchem ya maji ya chumvi.

2.2.1 Mahali ulipo Msitu na ukubwa wake

Msitu wa Kijiji cha Kisangi upo upande wa magharibi mwa ardhi ya kijiji. Unapakana na kitongoji cha Mikulyungu kwa upande wa mashariki, msitu wa kijiji cha Kikole kwa upande wa Magharibi, mto matandu kwa upande wa kusini na Kijiji cha Nambondo kwa upande wa kaskazini. Angalia Kiambatisho A: Ramani inayoonyesha mipaka ya kijiji na ya msitu na ramani shirikishi ya kijiji. Msitu upo katika eneo ambalo lilikuwa ni ardhi ya Kijiji cha Kikole lakini makubaliano yalifanyika kati ya pande zote mbili na Kijiji cha Kikole kiliridhia kukabidhi eneo la msitu ili lisimamiwe na kijiji cha Kisangi.

Msitu una ukubwa wa hekari 2,032.

Msitu unafikika kwa kupitia njia mbili toka shule ya msingi Kisangi. Njia ya kwanza kupitia kitongoji cha Mikulyungu na ya pili kupitia daraja la mipingo kupitia mtaa wa Naimba na msitu wa chanzo cha maji cha Mkwinda. Msitu uko umbali wa kilomita sita toka kijijini.

2.2.2 Uoto wa asili na Mazingira.

Eneo kubwa la msitu ni tambarare na uoto wa miombo (mataji wazi). Ramani shirikishi iliyoandaliwa na Kamati ya Maliasili ya Kijiji cha Kisangi inayoonyesha mahali zilipo rasilimali na meneo muhimu imeonyehwa katika Kiambatisho A.

2.2.3 Rasilimali za misitu.

Kabla ya kuvuna jamii yeyote ya miti iliyoorodheshwa, lazima tathmini ifanyike ili kubaini kiasi kilichopo na mpango wa uvunaji utatayarishwa. Tathmini ya kina itafanyika kufuatana na mwongozo wa Tathmini Shirikishi ya rasilimali za misitu uliotolewa na Idara ya Misitu na Nyuki katika Wizara ya Maliasili na Utalii. Taarifa za Tathmini shirikishi zimeambatanishwa katika mpango huu.

Mpango wa uvunaji utaelezea namna kiwango cha uvunaji kilivyopatikana kutokana na matokeo ya tathmini na utabainisha ni kwa namna gani kiwango hicho ni endelevu. Mpango wa uvunaji ni lazima upitishwe na kamati ya maliasili na kuambatanishwa katika mpango huu.

Jamii zote za miti zitavunwa kiendelevu, mbali na jamii za miti zilizoorodheshwa hapa chini hakuna jamii yeyote ya miti itavunwa kwa ajili ya biashara katika kipindi chote cha utekelezaji wa mpango.

2.2.4 Jamii za miti ya mbao

Kuna aina nyingi za jamii tofauti za miti ya mbao kama vile mvule, mpingo, mninga, mndundu, msufipori, mkongo, mkangazi, mtondoo, mkungutanga, mlipadeni/mwembeti, mpangapanga, mnyamwezi na mnangu

2.2.5 Mazao yasio timbao

Kuna aina mbalimbali za mazao yasiyo timbao kama vile mianzi, fito, nyasi, kamba, matunda, asali, ulanga, uyoga, nyama, anga na unyanya.

Miti inayofaa kwa ujenzi ni msenjele, msagawi, mtachi na mkaa na mingineyo. Miti ya matunda ni Mtopetope, Mtoe, Mkwaju, Msofu, Mndawa, Mgongo, Mfulu, Mbuyu, Mbinji, Ngombe na Mawilu.

2.2.6 Wanyama pori.

Wanyama pori wanaopatikana katika msitu huu ni Nyani, tumbili, Kima, Sungura, mbwamwitu, Bweha, Fisi. Simba. Kakakuona, Mhanga, Tembo, Nuruwepori, Ngiri, Nyati na wengineo. Matumizi ya Msitu

2.2.7 Mambo ya asili & Haki za kijadi

Kaburi la Mpumbe linatumika kimila. Wenyeji hutoa hela-sarafu kulingana na uwezo na endapo huna unaweza kutoa tumbaku kuanzia ujazo wa kikete kimoja kwa ajili ya kupata mahitaji mbalimbali kama nyama, kuvua samaki na kupata miti ya mbao na majengo.

2.2.8 Historia ya nyuma

Kuna baadhi ya maeneo ndani ya msitu yalitumika kama makazi ya watu wachache na mashamba yao kwa siku za nyuma. Pia uvunaji kwa ajili ya miti ya mbao na matumizi mengine ulifanyika.

2.2.9 Matumizi ya sasa

Watu huwa wanakwenda kwenye maeneo hayo ya msitu kupata asali, kukata majengo, mianzi ulanga, unyanya, angai na dawa za asili.

SURA YA TATU

3: MWONGOZO WA MATUMIZI YA MAZAO YA MISITU

Msitu utasimamiwa kama msitu wa asili na kutakuwa na mabadiliko kiasi katika usimamizi huo ili kuepuka kubadilisha hali ya uasilia wa msitu. Taratibu za kuingia msituni na za matumizi ya mazao ya msitu yameelezewa katika sura ya nne. Wale ambao hawatafuata taratibu hizi watapigwa faini au kuchukuliwa hatua za kisheria kulingana na sheria ndogo za msitu huu.

3.1 Matumizi ya msingi

Yatafanyika mawasiliano na kibali maalum kutoka kwa Serikali ya Kijiji na Kamati ya maliasili kitatolewa kwa wanajamii wa kijiji cha Kisangi kuingia katika Msitu wa Kijiji kupata matumizi ya msingi na kupita njia zinazofahamika. Taratibu hizi zitatumika pia kwa vijiji jirani vya Ruhatwe, Nambondo, Matandu na Kikole.

3.2 Matumizi huru ya msitu

Matumizi huru kwa wanakijiji wa Kisangi yatakuwa kwa ajili ya mazao yasio timbao kama vile uyoga, matundapori, mbogamwitu, kuni, nyasi, madawa ya asili na kutundika mizinga katika msitu wa kijiji. Vyote hivyo vitapatiwa kibali maalum cha bure toka kamati ya maliasili kwa kushirikiana na mwenyekiti wa kitongoji. Watumiaji wa nje ya kijiji wanaotaka kuvuna mazao haya kwa ajili ya biashara wanaweza kutozwa ushuru kama ilivyopangwa na Kamati ya Maliasili.

Wasio wakazi wa kijiji cha Kisangi wanaweza pia kuomba kibali toka kamati ya maliasili ya kijiji kutumia mazao yaliyotajwa hapo juu toka Msitu wa Kijiji. Kamati ya maliasili itakuwa na jukumu la kuhakikisha kuwa matumizi endelevu ya mazao haya yanazingatiwa.

3.3 Shughuli katika misitu zitakazotozwa ushuru

Shughuli zifuatazo zitatozwa ushuru na serikali ya kijiji ni:

- Kutembelea msitu kwa ajili ya mafunzo.
- Utafiti.
- Utalii msituni.
- Uvunaji wa miti kwa matumizi mbalimbali
- Uvunaji wa mazao yasiotimbao kwa ajili ya biashara

Viwango vya ushuru vimeonyeshwa katika Kiambatisho C. Wataalam na wawezeshaji hawatahusika na kutozwa ushuru.

3.4 Mazao yanayohitaji vibali vya uvunaji

- Miti ya mbao
- Asali
- Magogo
- Mianzi
- Majengo
- Uyoga

3.4.1 Utaratibu wa kupata leseni ya uvunaji

Utaratibu huu utahusisha miti yote iliyoorodheshwa katika kipengele 2.2.4 juu.

1. Mtu yeyote anayetaka kuvuna mazao ya misitu toka Msitu wa Kijiji lazima kwanza aandike barua ya maombi kijijini na aonyeshe aina na kiasi anachotarajia kuvuna.
2. Kamati ya Maliasili ya Kijiji itajadili na kupitisha ombi hilo endapo itaridhia kufuatana na matakwa ya mpango wa usimamizi na mpango wa uvunaji. Kama mpango wa uvunaji haujaandaliwa kibali hakitatolewa na uvunaji hauruhusiwi.
3. Kama haijaainishwa katika mpango wa uvunaji, Kamati ya Maliasili itapanga bei ya kuvuna mazao ya misitu na bei hizo kupitishwa na Serikali ya Kijiji.
4. Mwombaji atalipa gharama za leseni na kupatiwa stakabadhi halali.
5. Mwombaji atawasilisha stakabadhi ya malipo kwa Afisa Misitu wa Wilaya ambaye atampatia leseni ya kuingia msituni na kuvuna zao lililokubaliwa.
6. Mwombaji atarudi tena kijijini na kuwasilisha leseni kijijini, Kamati ya Maliasili itamwonyesha eneo la kuvuna mazao ya misitu anayoyahitaji.
7. Baada ya kuvuna magogo yote yaliyokatwa na visiki yatagongwa nyundo ya kijiji.
8. Mwisho mwombaji lazima apate kibali cha usafiri toka kwa Afisa Misitu Wilaya ili aweze kusafirsha mazao yake bila usumbufu nje ya Wilaya. Kibali hiki hutolewa bure na lazima kiwasilishwe kwa Afisa Mtendaji wa Kijiji ambaye ataweka kumbukumbu ya nambari ya kibali kabla mzigo haujatolewa kijijini.

3.5 Matumizi yasiyoruhusiwa ndani ya msitu

- Kilimo ndani ya msitu.
- Malisho ya mifugo ndani ya msitu.
- Makazi ndani ya msitu.
- Uvunaji wa miti ya mbao ambayo haijaorodheshwa katika kipengele 2.2.4 juu au miti ambayo haijatengenezewa mpango wa uvunaji.
- Kuchoma moto ovyo.
- Uanzishwaji wa njia mpya zisizo rasimi ndani ya msitu.
- Uzalishaji mkaa.
- Uchimbaji mdogo wa madini.

SURA YA NNE

4: HAKI, MANUFAA NA MAJUKUMU YA WADAU

Msitu wa kijiji cha Kisangi una wadau wafuatao; Serikali ya Kijiji, Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa na serikali kuu. Majukumu ya kila mdau yameelezewa kama ifuatavyo:

4.1 Kijiji

4.1.1 Haki

- Kumiliki na kutunza msitu wa Kijiji cha Kisangi.
- Kukamata, kupiga faini au kumshitaki mtu yeyote anayeenda kinyume na sheria ndogo za kijiji.
- Kutumia rasilimali kama ilivyobainishwa katika mpango wa Usimamizi wa Misitu.
- Kukusanya na kutumia ushuru na mapato mengine yatokanayo na mazao ya misitu katika shughuli za maendeleo ya jamii na hivyo kuboresha hali za maisha ya wanajamii.
- Kufanya maamuzi juu ya usimamizi na matumizi ya msitu.

4.1.2 Manufaa

- Kutumia miti na mbao kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa huduma za jamii kijijini.
- Mapato yatokanayo na faini na ushuru wa mazao ya misitu ingawa Halmashauri ya Wilaya inaweza kupewa mgawo kama ilivyoelezwa katika kipengele cha 6.2.
- Kupata mafunzo ya kitaalam katika masuala mbalimbali.

4.1.3 Majukumu ya Serikali ya Kijiji

- Msimamizi mkuu wa shughuli zote za utunzaji wa msitu.
- Kuthibiti mapato na matumizi yote yatokanayo na msitu.
- Kutatua migogoro inayohusiana na misitu pale inapojitokeza na kupeleka matatizo hayo ngazi ya Halmashauri ya Wilaya pale yanaposhindikana kutatua.
- Kuzuia uvunjwaji wa sheria.
- Kuhakiki vibali vyote vya uvunaji wa mazao ya misitu.vilivyotolewa na kamati ya Maliasili.
- Kupokea taarifa za uharibifu wa msitu toka Kamati ya Maliasili na wanajamii na kuzifanyia kazi.
- Kujadili na kupitisha mipango kazi ya mwaka ya Msitu wa Kijiji iliyoandaliwa na Kamati ya Maliasili.
- Kujadili na kuidhinisha matumizi yote ya fedha kwa Kamati ya Maliasili, doria na wajumbe wa Serikali ya Kijiji kwa ajili ya shughuli za msitu.

4.1.4 Majukumu ya Kamati ya Maliasili

Kamati ya Maliasili ina majukumu yafuatayo:

- Kuratibu shughuli zote za msitu kama vile; upandaji miti, ukusanyaji wa mazao ya misitu na kutunza kumbukumbu za msitu.
- Kutoa vibali vya uvunaji wa mazao ya misitu.

- Kuhakikisha doria imefanyika kila mara na kwa uhakika.
- Kufanya tathmini ya mazao ya misitu na kuandaa mpango wa uvunaji.
- Kuandaa mpango wa kazi wa mwaka wa shughuli za msitu..
- Kutoa taarifa za maendeleo na uharibifu wa msitu kwa serikali ya kijiji.
- Kuratibu shughuli zote zinazofanyika msituni.
- Kusimamia na kufuatilia uvunaji.
- Kupendekeza na kusimamia sheria ndogo.
- Kuijulisha jamii juu ya matukio katika Msitu wa Kijiji na maeneo yanayozunguka.
- Kuielimisha jamii juu ya mabadiliko ya miongozo mbalimbali ya utunzaji misitu.
- Kutoa taarifa ya robo, nusu na mwaka juu ya utekelezaji wa shughuli za usimamizi wa misitu kwa Afisa Misitu wa Wilaya.
- Kutoa taarifa ya robo mwaka kwa Halmashauri ili kuendana na utaratibu mpya wa kuweka kumbukumbu (NAFOBEDA).
- Kubuni mbinu mbalimbali za kuongeza kipato kama vile kutngeneza vinyago, ufugaji wa nyuki, ususi, ufinyanzi na vitalu vya miti.

4.1.5 Majukumu ya Wanakijiji

- Kuzuia uharibifu wowote utakaojitokeza katika msitu kama vile uchomaji moto na uvunaji holela wa mazao ya misitu.
- Kutoa taarifa ya uharibifu wa aina yeyote utakaofanyika ndani ya msitu kwa Kamati ya Maliasili na serikali ya Kijiji.
- Kushiriki katika shughuli zote za kuboresha msitu.
- Kupitia na kuidhinisha inapofaa sheria ndogo zilizopendekezwa na Kamati ya Maliasili.
- Kushiriki katika doria za kulinda msitu mara kwa mara.

4.2 Halmashauri ya Wilaya

4.2.1 Haki

- Kupokea taarifa za nusu mwaka juu ya utekelezaji wa shughuli za usimamizi wa msitu.
- Kukagua vitabu vya mapato na matumizi na kuchukua hatua zinazotakiwa kama italazimu.
- Kurudisha mamlaka ya usimamizi wa msitu chini ya halmashauri ya wilaya kama kijiji kitashindwa kuusimamia ipasavyo.

4.2.2 Manufaa

- Kupungua kwa gharama za usimamizi wa misitu.
- Kuboresha uhifadhi wa misitu.
- Kupungua kwa migogoro na migongano inayohusiana na matumizi ya misitu kati ya Halmashauri ya Wilaya na jamii.

4.2.3 Majukumu ya Halmashauri ya Wilaya

- Kuingilia kati kama kuna jambo au shughuli yeyote imefanyika kinyume cha utaratibu wa mpango kazi.

- Kutoa watalaam kwa ajili ya shughuli za msitu pale inapohitajika.
- Kusaidia kutafuta soko la mazao ya misitu.
- Kusimamia na kutatua migogoro ambayo iko juu ya uwezo wa serikali ya kijiji.
- Kuongoza zoezi la kubaini fursa na vikwazo.

4.3 Majukumu ya Serikali Kuu

- Kutoa watalaam washauri pale wanapohitajika.
- Kutoa miongozo mbalimbali inayohusu usimamizi misitu.

SURA YA TANO

5: SHUGHULI ZA KUENDELEZA NA KUTUNZA MSITU

Kutokana na msitu kuwa uoto wa aina moja, msitu mzima utakuwa na eneo moja la usimamizi. Mikakati ya jumla ya kutunza na kuendeleza msitu pamoja na rasilimali zake imewekwa bayana. Mambo yatakayoangaliwa ni upandaji wa miti na utunzaji wa machipukizi dhidi ya moto, ulinzi wa msitu, kinga na uthibiti wa moto pamoja na mpango wa matumizi endelevu wa mazao ya msitu. Mwongozo wa mpango wa utekelezaji wa miaka mitano umeonyeshwa katika Kiambatisho B.

5.1 Mikakati ya jumla ya kuendeleza msitu.

Katika kuendeleza msitu, mikakati ya jumla itakayofanyika ndani ya msitu ni kama ifuatavyo:-

- Kuthibiti aina yoyote ya kilimo ndani ya msitu.
- Kuthibiti uchomaji moto ovyo msituni.
- Kuthibiti malisho ya mifugo msituni.
- Kufanya doria za mara kwa mara ili kuthibiti uvunaji holela na uharibifu mwingine wa msitu.
- Kusafisha mipaka ya msitu na kuchimba mashimo ya mwelekeo kwa kila kona ya mpaka.

5.2 Ulinzi wa msitu

Usimamizi wa Msitu wa Kijiji utakuwa chini ya serikali ya kijiji na utatunzwa na wanajamii.

5.2.1 Ushirikishwaji wa jamii katika ulinzi wa msitu.

Msitu utalindwa na jamii kuzingatia mipaka yake, kila mtu atatoa taarifa kwa uongozi wa kijiji au kamati ya maliasili au kikosi cha doria pale anapoona uharibifu katika msitu. Kamati ya maliasili itaratibu na kusimamia shughuli za doria.

5.2.2 Walinzi wa doria

Kutakuwa na timu ya doria itakayochaguliwa na mkutano mkuu wa kijiji ambayo itakuwa na jukumu la kufanya doria za mara kwa mara katika Msitu wa Kijiji. Kikosi cha doria kitakachokuwa kama ifuatavyo:-

- Kamanda mmoja wa kikosi
- Wajumbe wawili wa Kamati ya Maliasili.
- Wanajamii watatu wenye uelewa wa masuala ya misitu

Doria inaweza kuwa ya wanakikosi wawili hadi sita, na kila doria lazima awepo mjumbe mmoja wa kamati ya maliasili, na mwanajamii mmoja. Kikosi cha doria kitaweka kumbukumbu zote za doria katika kitabu cha doria na kitatoa taarifa za matukio kwa kamati ya maliasili baada ya doria. Doria itafanyika angalau mara moja kwa wiki. Wanadoria watalipwa posho kutokana na makubaliano yatakayofanyika.

Kikosi cha doria kitachaguliwa na mkutano mkuu wa kijiji. Kamanda wa kikosi cha doria atakuwa na sifa zifuatazo; mtu shupavu ambaye ni mwaminifu. Wanakikosi watabadilishwa na mkutano mkuu wa kijiji kila baada ya miezi sita au wakati wowote inapobidi kufanya hivyo.

Wanakikosi cha doria watakaobainika kutokuwa waaminifu watafukuzwa mara moja na wengine watachaguliwa kujaza nafasi zao.

5.3 Kusafisha mpaka na barabara za moto

Kamati ya maliasili ya kijiji na jamii kwa ujumla watashiriki katika kusafisha mpaka wa msitu na kutengeneza barabara za moto. Kamati ya maliasili itaamua wapi barabara za moto zipite baada ya kupata ushauri toka kwa Afisa Misitu wa Wilaya.

SURA YA YA SITA

6: MAPATO NA USIMAMIZI WA MAZAO YA MSITU

6.1 Vyanzo vya mapato

Kutakuwa na vyanzo vya mapato vifuatavyo toka Msitu wa Kijiji:

- Ushuru.
- Uvunaji wa mazao ya misitu kwa ajili ya Biashara.
- Ada za leseni.
- Ada za vikundi vilivyoko mafunzoni, shughuli za utafiti na utalii.
- Na mengineyo kama vile faini za wahalifu n.k.

6.2 Mgawanyo wa Mapato kwa Wadau

Mgawanyo wa mapato yatokanayo na mazao ya msitu utakuwa kati ya Serikali ya kijiji na Halmashauri ya Wilaya. Mgawanyo huu utazingatia nani mwenye majukumu makubwa zaidi katika kutunza na kuendeleza msitu. Asilimia 10 inayotokana na mapato ya mazao ya msitu itapewa Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa kutokana na huduma inazotoa, Asilimia 90 itabaki kijijini. Hivyo hivyo katika serikali ya kijiji alimia 60 ya mapato yaliyotokana na maliasili yataelekezwa kwa serikali ya kijiji na asilimia 30 itapewa kwa kamati ya maliasili.

Matumizi ya mapato

Mapato yatokanayo na msitu yataelekezwa katika shughuli za:

- Kuendeleza shughuli za msitu zilizopangwa katika mpango kazi wa mwaka.
- Mapato yatakayobaki yatapelekwa kwa serikali ya kijiji ili yatumike katika shughuli za jamii.

Matumizi halali ya mapato yatokanayo na Msitu wa Kijiji ni:

- Kulipa motisha (posho) kwa doria.
- Vifaa muhimu kwa ajili ya kuendeleza shughuli za msitu kama ilivobainishwa katika mpango kazi wa mwaka.
- Matumizi mengine ya ziada ya kuendeleza msitu yaliyoidhinishwa na Serikali ya Kijiji.
- Ununuzi wa vitabu kwa ajili ya kutunzia kumbukumbu za shughuli za msitu.
- Kuchangia katika shughuli za maendeleo kijijini.
- Asilimia 30 ya mapato yatakuwa kwa ajili ya shughuli za usimamizi wa msitu chini ya Kamati ya Maliasili ya Kijiji.

6.3 Ukusanyaji na Utunzaji wa Fedha

- Serikali ya Kijiji pamoja na Kamati ya maliasili itahusika na ukusanyaji wa mapato.
- Serikali ya kijiji na mkuatano mkuu ndio wataidhinisha matumizi ya mapato.
- Kamati ya maliasili na kamati ya fedha na mipango ya kijiji itasimamia utunzaji wa mapato benki

Fedha zote zitatunzwa benki isipokuwa kwa fedha chache kwa ajili ya matumizi madogodogo. Pesa ndogondogo haitakiwi kuzidi shilingi 50,000/-. Kutakuwa na akaunti benki itakayo-funguliwa kwa jina la Mwembe ndawile. Kutakuwa na watia sahihi wanne; Afisa Mtendaji wa Kijiji (A), Mjumbe mmoja wa Kamati ya Mipango ya Kijiji (A), Mwenyekiti wa Kamati ya

Maliasili (B) na mweka Hazina (B) wa Kamati ya Maliasili ya kijiji. Mtia sahihi mmoja wa A na mmoja wa B watahitajika kuchukua pesa toka benki.

6.3.1 Vitabu muhimu vya kutunza kumbukumbu vinavyotakiwa

Mweka Hazina wa Kamati ya Maliasili atakuwa na jukumu la kutunza vitabu vya kumbukumbu. Vitabu vitakaguliwa na;

- Kamati ya fedha na mipango ya serikali ya kijiji.
- Mkaguzi wa ndani wa Halmashauri ya Wilaya.

Vitabu vitakavyokaguliwa ni;

- Jalada la kumbukumbu/muhitasari wa vikao.
- Kitabu cha kumbukumbu za doria.
- Kitabu cha kumbukumbu za uhalifu.
- Vitabu vya vibali na leseni.
- Kitabu cha stakabadhi za malipo yote yaliyofanyika kulingana na mpango kazi huu.
- Kitabu cha matumizi madogo madogo kwa ajili ya kumbukumbu za matumizi ya pesa ambazo hazikuwekwa katika akaunti ya benki.
- Kijiji kitatakiwa pia kutoa taarifa ya robo mwaka kwa Halmashauri ili kuendana na utaratibu mpya wa kuweka kumbukumbu (utaratibu huyo unaitwa NAFOBEDA kwa kitaalamu).

6.3.2 Taarifa ya Mapato na Matumizi

Kamati ya Maliasili itatoa taarifa ya Mapato na Matumizi kila mwezi kwa Serikali ya Kijiji. Pia kila baada ya miezi mitatu Serikali ya Kijiji itatoa taarifa za Kamati ya Maliasili katika mkutano mkuu wa kijiji ambapo Kamati ya Maliasili nayo itawakilisha taarifa.

6.3.3 Kuwajibishwa

Mwanakamati au mwanakijiji yeyote atakayepatikana na kosa la kutumia vibaya fedha za msitu atawajibishwa na serikali ya kijiji au atashitakiwa katika Baraza la usuluishi la kata au Mahakama ya mwanzo. Mjumbe yeyote wa Kamati ya Maliasili atakayepatikana na kosa lazima ajiuzulu haraka na atatozwa faini ya shilingi 50,000/- na uchaguzi mpya utafanyika kumchagua mjumbe mwingine kuziba pengo hilo.

SURA YA SABA

7: UFUATILIAJI NA TATHIMINI

7.1 Ufuatiliaji

Serikali ya Kijiji itafuatilia shughuli zote zilizopangwa kulingana na mpango kazi wa kila mwaka katika kipindi chote cha miaka mitano. Ufuatiliaji huu utahakikisha kuwa shughuli zote zimefanyika kulingana na mpango kazi.

7.2 Tathimini ya kati na ya mwisho

Zoezi la kubaini fursa na vikwazo litafanyika ili kuelewa hali ya maendeleo kama ilivyobainishwa katika mpango kazi huu. Zoezi hili litafanyika mwishoni mwa mwaka wa tatu , na mwishoni mwa kipindi cha miaka mitano.

Tathimini itafanyika kama ilivyoonyeshwa katika jedwali la utekelezaji wa mpango kazi lililoonyeshwa katika Kiambatisho B : Zoezi hili la tathmini litaongozwa na Afisa Misitu wa Wilaya chini ya mpango wa kitaifa wa Usimamizi Shirikishi wa Misitu.

VIAMBATISHO

KIAMBATISHO A : RAMANI ZA KIJIJI NA MSITU

Ramani inayoonyesha mipaka ya Kijiji

Ramani hapo juu inayoonyesha mipaka ya Kijiji cha Kisangi. Vijiji vinavyopakana na Kisangi vimeonyeshwa, mawe ya mipaka yameonyeshwa kwa alama ya pembetatu na kupewa nambari. Vipimo vya jiwe nambari 8 lililozungushiwa duara havikuchukuliwa wakati wa upimaji na vinafanyiwa kazi. Vipimo vya GPS (UTM37L : WGS84) katika mawe ya mipaka ni kama ifuatavyo;

Namba	Nambari ya utambulisho	E (m)	N (m)
1	SR295	516682	9032490
2	SR297	515999	9033321
3	SR298	513737	9038345
4	SR299	513611	9038834
5	SR306	514334	9040438

Namba	Nambari ya utambulisho	E (m)	N (m)
6	SR211	515026	9041004
7		516953	9041224
8	VB5(NP)	516852	9046627
9	VL100	519931	9044066
10	SR293	524588	9041597
11	SR292	524026	9039049
12	SR291	523984	9037103
13	SR290	523667	9036186
14	SR289	523973	9034761
15	SR287	524572	9033843
16	VB5B	517071	9030403
17		517118	9032417

Ramani inayoonyesha mipaka ya Msitu wa Kijiji



Ramani hapo juu inayoonyesha mipaka ya Msitu wa Kijiji cha Kisangi. Mawe ya mipaka yameonyeshwa kwa alama ya pembetatu na kupewa nambari. Vipimo vya GPS (UTM37L : WGS84) katika mawe ya mipaka ni kama ifuatavyo;

Namba	Nambari ya utambulisho	E (m)	N (m)
1	SR295	516682	9032490
2	SR297	515999	9033321
3	SR298	513737	9038345
4	SR299	513611	9038834
5	SR306	514334	9040438
6	SR211	515026	9041004
7		516967	9041226
8		517119	9032417

Ramani Shirikishi ya Kijiji

Ramani hii iliandikwa na wanakijiji wa Kisangi.

KIAMBATISHO B : MPANGO WA UTEKELEZAJI

Kazi za kila mwaka

- Doria za mara kwa mara.
- Kubabua moto.
- Kusimamia matumizi ya sheria ndogo (Serikali ya Kijiji).
- Kuweka kinga za moto (Kamati ya maliasili).
- Ulinzi wa Msitu (jamii nzima).
- Kukusanya mapato yatokanayo na mazao ya misitu (Kamati ya maliasili).
- Kusafisha mipaka kuzunguka msitu (Jamii na Kamati ya maliasili).

Kazi za Mwaka wa Kwanza

- Kujenga kituo cha ukaguzi wa mazao ya misitu (Kamati ya maliasili).
- Kupaka baadhi miti iliyoko mpakani rangi ili mipaka ielewe vizuri. Kusini (Mchanga mzuri), Kaskazini.
- Kufyeka mpaka na kuchimba mashimo kwenye kona za mpaka.
- Tathimini ya miti iliyo tayari kuvunwa.

Kazi za Mwaka wa Pili

- Kufyeka barabara za moto.
- Kufyeka mpaka wa msitu na kufukua mashimo.
- Upandaji wa miti kwa maeneo yaliyo wazi.

Kazi za Mwaka wa Tatu

- Upandaji wa miti kwa maeneo yaliyo wazi.
- Kufyeka mpaka wa msitu.
- Kufanya tathimini ya mafanikio ya mpango wa usimamizi wa msitu wa kijiji.

KIAMBATISHO C : VIWANGO VYA USHURU

- Makundi ya mafunzo yatakayotembelea msitu yatatozwa shilingi zisizozidi 10,000/- kwa kikundi.
- Watafiti kila mmoja atalipa shilingi zisizozidi 3,000/- na taarifa ya utafiti kurudi kijijini na zinatakiwa ziwe katika lugha ya Kiswahili.
- Watalii watalipa shilingi 10,000/- kwa siku kwa kichwa.
- Waongoza watalii na wageni watalipwa shilingi 5,000/- kwa siku kwa kichwa.